

Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.

Uje Roho Mtakatifu uzienee nyoyo za waamini wako uwashe mapendo yako peleka Roho wako vitaumbwa upya na nchi zitageuka. Tuombe. Ee Mungu uliyezifundisha nyoyo za waamini ukiwaletea mwanga wa Roho Mtakatifu tunaomba utuongoze na yule Roho tupende yaliyo mema tupate daima faraja zake tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

Tuusifu Utatu Mtakatifu kwa Mungu sasa na siku zote na milele. Amina.

Ewe Utatu Mtakatifu kwa Mwenyezi Mungu Baba Mwana na Roho Mtakatifu nasadiki kuwa uko hapa na pahali pote Ee Mungu wangu umeniumba, umenikomboa, umenifanya mkristo umenizidishia na neema zako umenitayarishia makao yangu uwinguni, umenijalia na siku nikutumikie Ee Mungu nakuabudu nakuheshimu nakuomba toba nakupenda Ee Mungu nakutolea Roho yangu na mawazo na maneno na kazi na furaha na mateso yangu yapokee unipe neema yako nisitende leo dhambi.